# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## MAMLAKA YA VYUO VYA UFUNDI (NACTVET)
# KILITECH VOCATIONAL TRAINING CENTRE

**Tovuti: www.kilitechcollege.ac.tz**
**Barua pepe:** info@kilitechcollege.ac.tz
**Simu:** 0759 538060, 0766978511, 0621793493
**S.L.P 252**
**MPANDA-KATAVI.**

**USAJILI : REG/NACTVET/0903**

Tarehe: 20/01/2025

**MZAZI/MLEZI WA**: **……………………………………………………….**
NAMBA YA MTIHANI: ______________________

**YAH: KUKUTAARIFU KUWA UMEKIDHI VIGEZO VYA KUJIUNGA NA MAFUNZO KATIKA CHUO CHA KILITECH KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026.**

1. Uongozi wa chuo cha **KILITECH ,** kupitia Mamlaka ya Vyuo vya Ufundi Stadi (NACTVET) tunayo furaha kukufahamisha kuwa kwa ufaulu ulio upata kwenye matokeo yako kidato cha nne umekidhi kujiunga na mafunzo ya chuo katika kozi **MOJAWAPO KATI YA ZIFUATAZO**:-
   i) **INFORMATION & COMMUNICATION TECHNOLOGY (ICT)** kwa ngazi ya Astashahada (cheti) miaka 2 hadi 3 (NVA LEVEL II hadi NVA LEVEL III)
   ii) **ELECTRICAL INSTALLATION (UFUNDI UMEME)** kwa ngazi ya Astashahada (cheti) miaka 2 hadi 3 (NVA LEVEL II hadi NVA LEVEL III)
   iii) **EARLY CHILDHOOD EDUCATION (UALIMU WA AWALI, MALEZI NA MAENDELEO YA WATOTO)** kwa ngazi ya Astashahada (cheti) miaka 2.
2. Chuo kinamilikiwa na kampuni ya **Kilitech Solutions**, kinasimamiwa na serikali na kimesajiliwa na **NACTVET** kwa usajili wa kudumu namba **REG/NACTVET/0903.**
3. Chuo kipo Mkoani Katavi wilaya ya Mpanda (mjini) 3km kutoka Mpanda mjini barabara ya Sumbawanga kituo cha kushukia ni stendi mpya ya mkoa iitwayo Mizengo Pinda Bus Terminal.
4. **Udahili/usajili wa wanafunzi utaanza tarehe 03/03/2025 hadi tarehe 18/03/2025.**
5. Mwanafunzi anatakiwa kuthibitisha kuwa ataripoti chuoni kwa njia ya simu baada ya kupokea barua hii. ***Zoezi la ujazaji fomu litafanyika baada ya mwanafunzi kuripoti chuoni au kupitia tovuti ya chuo***
6. Chuo kina hostel kwa ajili ya wanafunzi wa kike ambapo gharama ya hostel ni Tsh**15,000** kwa kila mwezi ambapo inalipwa kila baada ya miezi mitatu. Suala la chakula kwa wanaoishi hostel chuo kimetoa ruhusa ya wanachuo kujipikia chakula, Kwa watakao kosa nafasi za hostel chuo kinawajibika kuwatafutia vyumba vya kupanga maeneo ya chuo. Wavulana watatafutiwa vyumba vya kupanga kwani chuo hakina hostel za wavulana.
7. Mwanachuo kila baada ya muhula wa kwanza wa mwaka wa pili (semester one) anatakiwa kwenda field (PT) mafunzo kwa vitendo.
8. Baada ya mafunzo mwanachuo atakuwa na uwezo wa **kujiajiri**, **kuajiriwa serikalini** na **secta binafsi** (private sectors kama vile makampuni na mashirika mbalimbali).
9. Sare za chuo zinapatikana chuoni isipokuwa viatu(vyeusi), sweta(blue), socks na tracksuit(dark blue) ya mazoezi ambapo mwanachuo atajinunulia pindi anapo ripoti chuoni.
10. Mwanachuo anatakiwa aje na Passport size mbili na rimu moja ya A4.
11. Mwanachuo atatakiwa kununua vitendea kazi vya ufundi ambavyo atavimiliki yeye mwenyewe na vitakuwa mtaji wa kuanzia amalizapo chuo kama vile (**Electrical/ICT Tool Kit**) n.k.
12. **Baadhi ya vipengele ambavyo viko ndani ya fani za ufundi ni:- Ufundi wa computer, ufundi wa umeme wa majumbani na viwandani, fensi za umeme, umeme wa solar, ufungaji wa miundombinu ya internet, ufungaji wa camera za ulinzi, usanifu wa picha, kusanifu tovuti, mifumo mbalimbali ya computer kama vile (Biometric system, BRELA, NEST, NIDA, Microsoft packages , NACTVET, HELSB) na mengine mengi.**

KILITECH VOCATIONAL TRAINING CENTRE

**ADA YA MAFUNZO NA GHARAMA ZINGINE KWA FANI (COURSE) ZA ICT, UMEME NA UALIMU WA AWALI.**

Ada ya chuo kwa mwaka ni **Tsh850,000/=**

**MTIRIRIKO WA MALIPO YA ADA NA MICHANGO MINGINEYO KWA MWAKA**

| | **March** | **June** | **September** | **December** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|
| **ADA** | **250,000** | **200,000** | **200,000** | **200,000** | **850,000** |
| **MICHANGO MINGINEYO** | **105,000** | **100,400** | **0** | **0** | **205,400** |

***N.B: Mwanafunzi alipie angalau 355,000/= ada na michango mingineyo kwenye akaunti ili aweze kupokelewa na kudahiliwa kama jedwali linavyoonesha hapo juu.***

UFAFANUZI WA GHARAMA YA MICHANGO MINGINEYO KUTOKEA JEDWALI LA JUU

| JINA LA MCHANGO | KIWANGO | MUDA WA KULIPA |
|---|---|---|
| Student ID (Kitambulisho) | 10, 000/= | Mwaka wa1 |
| Renovation (Ukarabati) | 15,000/= | Mwaka wa1 |
| Student Organization | 15,000/= | Mwaka wa 1 |
| Bima ya Afya kwa wasionazo | 50,400/= | Kila mwaka |
| Local Examination | 25,000/= | Mwaka wa 1 |
| Student uniform (trouser/ skirt, shirt, t-shirt, overcoat) | 60,000/= | Mwaka wa1 |
| Practical field and Research | 20,000/= | Kila mwaka |
| Rim paper | Aje na Rim | Kila mwaka |
| Application form | 10,000/= | Mwaka wa 1 |
| **Total (Jumla ya Gharama)** | **205,400/=** | |

**UTARATIBU WA KULIPA ADA NA MICHANGO MINGINEYO / REGULATION FOR PAYMENTS**

- Ada na Michango ilipwe kupitia Account NAMBA **015C551261100 C R D B**,
  JINA LA AKAUNTI NI: **Kilitech Vocational Training Centre**

NB: Malipo yote yafanyike Benki au kwa wakala wa CRDB kwa utaratibu ulioonyeshwa hapo juu ili kuepuka usumbufu wowote unaoweza kujitokeza.

- Baada ya kuonyesha risiti za benki kwa mhasibu wa chuo, hakikisha unapewa stakabadhi/risiti ya malipo ya chuo.

13. Mwanachuo anatakiwa aje na godoro la futi $2^{1}/_{2}$, na chandarua pamoja na vifaa vya usafi binafsi,
14. Hakuna fedha itakayorudishwa kwa mwanafunzi atakaeacha chuo, kuhama au kwa namna yeyote ile.
15. Chuo kina miundombinu mizuri ya kujifunzia kama vile (computer za kujifunzia, Internet ya bure (wifi) masaa 24, umeme na maji ya uhakika, na uwepo wa wakufunzi mahiri.
16. **WANACHUO WANAOHITIMU MAHALI HAPA WOTE WAKO KAZINI** (wamejiajiri, wameajiriwa → serikalini na sekta binafsi). Chuo pia kimekuwa kikiaminiwa na taaasisi mbalimbali hivyo wanachuo wahitimu wamekuwa wakipata fursa za kuajiriwa katika taasisi hizo. Chuo pia kimekuwa kikihusika kuwatafutia fursa mbalimbali wahitimu panapo uwezekano.

→ Tunakutakia maandalizi mema na safari njema, **karibu sana chuo cha Kilitech upate maarifa yatakayokuwezesha kujikomboa maishani mwako**.

**NB:** Mwanachuo anapofika stendi kuu ya mabasi (**Mizengo Pinda bus Terminal**) anatakiwa apige simu ili aje achukuliwe na usafiri wa chuo kuepusha gharama zisizokuwa za lazima.

BARAKA REDSON JECK
MKUU WA CHUO

KILITECH VTC PRINCIPAL MPANDA - CAMPUS

KILITECH VOCATIONAL TRAINING CENTRE